**LEARNING BY EAR 2012**

**"Wasaliti walo karibu – Hadithi inayoangazia dhulma zinazoambatana na ngono"**

**EPISODE 8: 'Simama'**

**AUTHOR: Chrispin Mwakideu**

**EDITOR: Andrea Schmidt, Pendo Paul**
**PROOFREADER: Pendo Paul**

**List of characters by scene:**

**<u>SCENE ONE: JUDY RETURNS TO MR. MANENO'S OFFICE</u>**

- **Pato (f, 16)**
- **Maneno (m, 45)**
- **Judy (f ,45)**
- **Narrator (m/f, around 30)**

**<u>SCENE TWO: ALLAN HAS A TOUGH TIME  AT SCHOOL</u>**

- **Allan (m, 10)**
- **Mrs. Rimba (f, 45)**
- **Boy (m, 10)**
- **Boys voices (m, 10-11)**

- **Narrator (m/f, around 30)**

**<u>SCENE THREE: PRECIOUS PAYS JOE A VISIT IN PRISON</u>**

- **Precious (f, 30)**
- **Joe (m, 45)**
- **Narrator (m/f, around 30)**

**<u>SCENE FOUR: JUDY WITH VICTIMS OF SEXUAL ABUSE AT CENTRE</u>**

- **Judy (f, 40)**
- **Nuru (f, 30)**
- **Mixed voices (women)**
- **Narrator (m/f, around 30)**

**UTANGULIZI:**

Nakusabahi na karibu katika kipindi chetu cha **Noa bongo, Jenga maisha yako**. Hiki ni kipindi cha nane katika hadithi inayoendelea ya, **'Wasaliti walo karibu'.** Iwapo ulipitwa na kipindi kilichopita, hii ni kumbukumbu yake: Dulu aliamua kumuacha mkewe Nuru, baada ya kutengwa na kubaguliwa na rafiki zake sababu kuu ikiwa ni kubakwa kwa Nuru na kundi la waasi. Pato, mwanafunzi wa kike alikuwa amueleze Judy yaliyokuwa yanamsibu, baada ya mkereketwa huyo kutembelea shule yao na kuwahamasisha dhidi ya dhuluma za kingono. Lakini Bw. Maneno, mwalimu mwenye kumdhulumu Pato, akamzuia kusema lolote. Judy akaondoka, lakini hakufika mbali akaamua kurudi shuleni baada ya kushuku uhusika wa Bw. Maneno katika unyanyasaji huo. Kwengineko, Uncle Joe anakamatwa na askari baada ya kijana wa miaka 10, Allan kumweleza mwalimu wake, Bi. Rimba kuwa yeye anamdhulumu kingono kwa kumlawiti. Kutatumbuka nini kwenye jipu hili? Tusubiri hatima ya kipindi hiki cha leo kwa jina, **'Simama'.** Tunafunguwa jamvi letu ofisini kwa Bw. Maneno, ambae kakasirishwa na Pato baada ya kutaka kumweleza Judy kuhusu dhuluma hizi.

**SCENE ONE: JUDY RETURNS TO MR. MANENO'S OFFICE**

1. **SFX: DOOR BEING CLOSED AND LOCKED**

2. **MANENO:** **(furious)** Pato! Umemueleza nini yule mwanamke mshenzi ? Hah?… Sikiliza – kama hunielezi, nitaamuru ufukuzwe hapa shule. Naweza kutumia cheo changu. Halafu mamako atasema nini?

3. **PATO:** **(makes frightened noises)**

4. **MANENO:** **(shouts at her)** Zungumza! Huna shukurani mtoto wewe! Hufurahii, nimekufanya ukaongoza darasani? Nimekupa mia kwa mia somo la Baiolojia, hata kama ulipata asilimia hamsini tu! Na malipo yako ni haya? Unanisaliti? Kuna haja gani ya kuwaambia watu siri yetu?

5. **PATO:** **(scared)** Lakini… laki.… Bw. Maneno… Si…

6. **MANENO:** **(softly)** Keti chini. …**(harshly, commanding)** Hutaki kuketi, Pato?

7. **PATO:** Tafadhali… Tafadhali usiniguse… **(about to start crying)** Bw. Maneno, sitaki kushikwa na wewe… Usithubutu! Usinishike…

8. **SFX: DOOR BEING BANGED HARD**

9. **JUDY:** **(screaming)** Fungua huu mlango! Bw. Maneno, nimesikia yote uliyomweleza Pato. Fungua huu mlango au niite polisi!

10. **SILENCE**

11. **JUDY:** **(calls out)** Pato! Uko salama?

12. **PATO:** **(still crying)** Ndiyo.. niko sawa.

13. **JUDY:** Haya. - Maneno, mambo kwisha. Tafadhali fungua mlango. Huu ni wakati wa kuvuna uhaini wako.

**14. SFX: DOOR BEING SLOWLY OPENED**

**15. MANENO:** Bi. Judy, nafikiri unakosea mahala. Sijui unafikiria nini kunihusu…

**16. JUDY:** Usijaribu kukanusha, mtazame ulivyomfanya! Pato, usijali – uko salama sasa. Vaa shati lako na uandamane nasi.

**17. MANENO:** **(begging)** Sawa.. sawa... sina nia yeyote ya kumdhuru... tafadhali nisameheni. Haina haja ya kuita polisi. Nihurumieni mimi. Nina mke na watoto. Mtawatesa bure, nawaomba.

**18. JUDY:** Ungelifikiria hilo kabla ya kuanza kudhulumu wanafunzi wako. Sijui ni wangapi kama yeye wamepitia mikononi mwako na wakashindwa kujieleza.

**19. MANENO:** La, ni Pato pekee, naweza kuapa kwa Mungu! Sijawahi tena hii ni mara ya kwanza na nishaacha. Nimekoma!

**20. JUDY:** Sidhani. Karibu unifanye mjinga, Maneno. Lakini haijalishi, leo ni mwisho wako! Maovu yote uliyomtendea utayalipa. Pato, hebu njoo. Hakuna tatizo; usiogope.

**21. MANENO:** Sawa, ninakubali – nilijua nafanya makosa, lakini nilishindwa kujizuia. Nisaidieni. Mnaweza kunisaidia, Bi. Judy. Tafadhali sitarudia tena nipeni nafasi nyengine ya pili.

**22. JUDY:** **(Angry)** Nafasi ya pili? Ya nini? Kuzidi kuwadhulumu wanafunzi? Sahau! Wewe ni mwalimu wake. Umeaminiwa uwafunze, sio kuwadhulumu na kuwafuja. Haya ni mambo ya polisi sasa.

**23. MANENO:** Polisi? La - tafadhali! Naomba msamaha!

**24. JUDY:** Haifai kitu. Nikitoka hapa mimi na Pato moja kwa moja naenda kupiga ripoti kituo cha polisi. Halafu sheria ichukuwe mkondo wake.

**25. MSIMULIZI:** Judy msimamo wake ni huo huo. Bw. Maneno analazimishwa kujiuzulu kama mwalimu. Mahakama inamsubiri na mashtaka makubwa. Unafikiri alivyotenda Judy ni sawa? Ama unafikiri wahalifu wa ngono wanastahili nafasi ya pili? Uking'amua swali hilo, sasa tumtembelee kijana Allan. Akiwa amerudi shuleni na tayari anaendelea na masomo yake ya kawaida; lakini, kama ilivyo kwa waathiriwa wa dhuluma hizi za kingono, kukubalika kwao na jamii huwa sio rahisi.

**SCENE TWO: ALLAN AKIWA NA WAKATI MGUMU**

**26. SFX: YOUNG SCHOOL BOYS LAUGHING AND JEERING**

**27. ALLAN:** Niache! Nitakusema kwa mwalimu Rimba.

**28. BOY:** **(mocks him)** Allan hana misuli… Allan hana nguvu…

**29. (OTHER BOYS JOIN IN CHORUS- 'Allan is a softy!')**

**30. RIMBA:** Wewe! Nyinyi! Wacheni uchokozi! Kwanini mnachokozana? Njooni hapa, nyote watatu! Kujeni haraka. Na Allan, pia wewe njoo, tafadhali. Ehe… Walikuwa wanakwambia nini, Allan?

**31. ALLAN:** Walikuwa wanasema eti mimi sina nguvu wala misuli.

**32. RIMBA:** Ni kweli? Na kwanini mnamuita mwenzenu Allan hivyo? Haraka, mnijibu. Kwanini mseme mvulana mwenzenu hana nguvu?

**33. BOY:** **(afraid)** Kwa sababu hataki kucheza na sisi, anaketi tu. Lakini tulikuwa tunafanya matani, mwalimu Rimba.

**34. RIMBA:** Sikilizeni, Nyinyi watatu, sitaki hayo matani yenu. Hayapendezi. Sasa nataka mumuombe msamaha, nikiwasikia tena au mkimkejeli tena, sitawahurumia. Mnasikia?

**35. BOYS:** **(timidly)** Ndiyo, Bi. Rimba…

**36. RIMBA:** Sasa muombeni Allan msamaha.

**37. BOYS:** Tusamehe, Allan.

**38. BOY:** Ukitaka njoo ucheze nasi.

**39. ALLAN:** Sawa.

**40. MSIMULIZI:** Watoto kama Allan hupitia mengi kabla ya uponyaji kamili kufika. Dhuluma zitokeazo katika umri mchanga, huwaondosha uaminifu, utangamano na watu, na kujitenga na watu. Ni muhimu kuwasaidia waathiriwa hawa – kwa kuwapa ushauri, kuwaelimisha, na kutumia makundi ya marika. Mwalimu Rimba anajaribu sana kumsaidia Allan, lakini anajua haitakuwa rahisi. Siku chache baadae Uncle Joe alifikishwa kortini, pamoja na ushahidi aliotoa Bi. Rimba na Allan mwenyewe, alipatikana na hatia na kufungwa miaka mitano taslimu. Siku baada ya hukumu hiyo kutolewa , Precious, mamake Allan, anamtembelea mpenzi wake wa kitambo.

## SCENE THREE: PRECIOUS PAYS JOE A VISIT IN PRISON

**41. SFX: PRISON AMBIENCE, IRON PRISON DOOR OPENS**

**42. JOE:** **(cheerful)** Hujambo mpenzi! Ni vyema kujua unatamani kuniona.

**43. PRECIOUS:** **(grinding her teeth in anger)** Mpenzi wa nani shetani ibilisi wewe! Mpuuzi, mkosa fadhila, mwehu wewe!

**44. JOE:** Precious, mpenzi wangu… yani unaamini yale mtoto wako aliyosema kortini? Ati mimi! Joe wako.

**45. PRECIOUS:** **(interrupting)** Funga domo lako chafu! Sitaki tena kuiona sura yako machoni pangu. Nilikuamini! Nilikutetea mbele ya mwalimu wa Allan, na kumbe wakati wote umekuwa ukiniharibia mtoto? **(remorseful)** Arrgh! Yani nilikuwa ni mjinga kiasi gani!

**46. JOE:** **(chuckle)** Sio kosa lako, Precious, hakuna anayeweza kuishi bila mimi. Lakini usijali – ni miaka mitano tu, na hata inaweza kupunguzwa nikiwa mtiifu gerezani, inaweza kuwa hata miwili alafu nitatoka tuje tuendelee na maisha…

**47. PRECIOUS:** Una uji badala ya ubongo kichwani! Akili yako ni timamu wewe? Una wazimu! Ilikuwaje hadi nikakuamini mpaka nikakuruhusu kuishi nyumbani kwangu? Nilikupenda sana, nilikugharamia mahitaji yako, na mwanangu ukamkosea kiasi hiki! Lakini sasa mambo ni tofauti, Joe. Sina haja ya kukuona tena! Nakuombea uozee huko jelani!

**48. JOE:** Aaah, usiseme hivyo, Precious… kweli unamaanisha hivyo? **(chuckles again)** kwani nimekuwa muovu kiasi hicho. Huwezi kuishi bila mimi! Hata wewe unajua hilo!

**49. SFX: PRISON DOOR BEING SHUT**

**50. MSIMULIZI:** Hatimae Precious anang'amua alikuwa akimuamini mtu asiyestahili kuaminiwa, na jawabu ni maafa kwa mtoto wake. Ni mnyonge na mwenye huzuni kubwa, sasa ameamua kumkinga Allan na madhara mengine yawayo. Siku iliyofuata, magazeti yote yalikuwa na vichwa vya habari ya kushikwa kwa Joe. Wengi waliosoma taarifa hizo waliona miaka mitano ni michache mno kwa makosa mengi na mazito kama hayo. Judy anasoma habari hizi akielekea kituoni mwake, anakofanyia ushauri waathiriwa wa dhuluma za kingono.

**<u>SCENE FOUR: JUDY AT THE CENTRE WITH VICTIMS OF SEXUAL ABUSE</u>**

**51. SFX: NEWSPAPER PAGES BEING SHUFFLED**

**52. JUDY:** **(furious)** Mimi siamini? Hii si haki kamwe! Inauma tena sana,… Hebu sikilizeni nyote: **(reads)** Mwanaume aliyemlawiti mvulana wa miaka 10 afungwa gerezani…. kwa miaka mitano.

**53. SFX: SHOCK / DISBELIEF REACTION FROM MOSTLY WOMEN**

**54. JUDY:** Subirini nimalize toleo...**(continues to read**) Kaimu mkuu amfunga mwanaume huyo kwa miaka mitano baada ya kupatikana na hatia ya kumlawiti mvulana wa miaka 10. Mwanamume huyo, aliyejulikana kama baba yake wa kambo amekuwa akimfanyia unyama huyo kijana kila wakati mamake alipokuwa amekwenda kazini. Muasi huyo hakuonyesha majuto wala kuathirika kwa lolote wakati adhabu hiyo ilipokuwa ikitolewa. Mashtaka ya jinsia na dhuluma za kingono yameongezeka nchini kama… **(breaks off)**

**55. SFX: NEWSPAPER RUFFLED AND SHUFFLED**

**56. JUDY:** Siwezi kuvumilia tena. Sheria za masuala ya dhuluma za kingono ni dhaifu nchini. Lazime zitiliwe uzito. Ili kulinda manusura na waathiriwa ni lazima serikali iunde sheria kali bungeni!

**57. SFX: LIGHT APPLAUSE**

**58. JUDY:** Nimeamua kuaandaa kongamano kubwa, na nyote nawaalika. Wengine mnaweza hata kueleza visa vyenu ilhali wengine mtakaa kimya, cha msingi ni kuhudhuria tu. Aliye tayari – nitakuwa naye wakati akihadithia mikasa yake. Ni wakati muafaka kuwaeleza viongozi wetu ukweli. Nani yu tayari? Nani atafichua ukweli?

**Silence**

**59. JUDY:** Nafurahi kuwa nanyi! Hamkuepuka tu bali, mlikuwa jasiri kutaka matibabu. Natumai wengine wataiga mfano wenu. Lakini kwanza tutafute kuungwa mkono. Hadithi zenu, zina uchungu na za kuogofya, zaweza kuleta mabadiliko. Serikali sharti isukumwe kuleta badiliko; pia tunataka waathiriwa wengine wasifikiri wako peke yao. Lazima tuangamize dhulma hizi!

Najuwa wengi mna subiri muda huo tu ufike mjieleze.

**60. NURU:** Mimi najitolea!

**HITIMISHO:** Na kwa hayo tunalifunga jamvi la kipindi hiki cha nane kwenye hadithi inayoangazia masaibu ya waathiriwa wa dhuluma hizi za kingono. Nuru amefika tu kituoni, lakini amevutiwa na wazo la kuwahamasisha wanawake wengine wajitokeze kusema ukweli katika kugandamiza dhuluma hizi. Anajitolea kusema kisa chake hadharani – lakini kweli anajua uzito wake? Litamfika lipi Pato, hivi ambavyo Bw. Maneno amejiuzulu kazi yake? Je,Judy atafaulu kuzijenga sheria zinazopinga dhulma hizi? Usikose kusikiliza kipindi kijacho... na usisahau kwa maoni na kusikiliza tena vipindi vyetu tembelea tovuti yetu dw.de/lbe. Au mtandao wa Facebook! Mpaka wakati mwengine – tuonane.